# Azimio la Hyères la Walinzi wa Pori, 2024

Kongamano la 10 la **Shirikisho la Kimataifa la Walinzi wa Pori (IRF)** kwa Walinzi wa Pori Duniani (WRC) mjini Hyères kuanzia tarehe 7 hadi 11 Oktoba, 2024 lililoandaliwa na IRF, pamoja na **Gardes Natures de France (GNF)**, lilihudhuriwa na walinzi wa pori na watetezi 450 (asilimia 49 wanawake na asilimia 15 watu wa Kiasili na Jumuiya za Maeneo) kutoka nchi 88. Kongamano la WRC linakamilika katika wakati muhimu kwa sayari yetu, kwani inakabiliwa na kufifia kwa bionuwai, kuongezeka kwa mabadiliko ya tabianchi na hatari kuzidi kupaa juu kutokana na magonjwa ya kuambukiza yanayoenea kati ya wanyama. Walinzi wa Pori, kama Wahudumu wa Afya ya Sayari[1], wanajua jukumu muhimu wanalopaswa kutekeleza katika kushughulikia majanga haya. Wamejitolea kufanya kazi na washirika ili kufikia malengo na kusudi letu la kimataifa na kuwezesha mabadiliko ya uchumi wa kijani. Hata hivyo, kufikia malengo haya kunasalia kuwa jambo lisilowezekana sana bila nguvukazi ya walinzi wa pori wenye taaluma, ufanisi, uwajibikaji na ushirikisho. Ili kuhakikisha utekelezaji wa haraka na bora wa malengo haya, sisi, wawakilishi wa nguvukazi ya walinzi wa pori na watetezi wa WRC ya 10 tunaidhinisha Azimio la Hyères la 2024 la Walinzi wa Pori kama ifuatavyo;

**KUANGAZIA** hatua zilizopigwa na Shirikisho la Kimataifa la Walinzi wa Pori (IRF) tangu Kongamano la 9 la Walinzi wa Pori Duniani la IRF kwa ushirikiano na washirika kama Muungano wa Usaidizi wa Walinzi wa Pori Ulimwenguni (URSA) na wengine wengi kutekeleza **Azimio la Chitwan** kupitia kuongeza uhamasishaji, kukuza viwango vya kimataifa na kutetea mahitaji ya walinzi wa pori kwenye jukwaa la kimataifa.

**KUKUMBUKA** Maazimio na Ahadi zilizopitishwa katika makongamano ya kikanda na mabaraza miongoni mwa mengine Baraza la Walinda Pori wa Asia (2023), Baraza la Walinda Pori wa Oceania (2023), Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Walinda Pori la Amerika Kusini (2024), Kongamano la Walinda Pori wa Afrika (2022) na Kongamano la Walinda Pori wa Ulaya ( 2023).

**KUKIRI** kwamba walinzi wa pori[2] ndio wasimamizi wakuu wa asili na urithi wa kitamaduni, wanaolinda rasilimali hizi kwa ajili ya vizazi vijavyo, na kukubali kwamba kuunga mkono kazi yao yenye thamani ni muhimu kwa kulinda hazina za kiikolojia na kitamaduni za sayari yetu kama wachangiaji muhimu kwa afya ya sayari.

**KUTAMBUA** kwamba walinzi wa pori ni kikundi kipana ambacho kina wingi wa mahitaji na vikwazo, kwa hivyo tunatambua kwamba mahitaji yao ya kibinafsi na ya pamoja ya usaidizi yanapaswa kushughulikiwa katika muktadha wa kitaasisi.

[1] https://www.researchgate.net/publication/372381236_Essential_planetary_health_workers_Positioning_rangers_within_global_policy

[2] https://www.internationalrangers.org/resource/code-of-conduct-english

Our funders

Institutional support

**KUTAMBUA** kwamba licha ya jukumu lao muhimu, walinzi wengi wanakosa vifaa vya msingi, mafunzo, idadi ya kutosha na ulinzi unaohitajika ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na usalama. Taaluma hii mara nyingi haipati kutambuliwa inavyostahili.

**KUKUBALI kwamba wengi wa** walinzi wa pori hufanya kazi katika mazingira magumu ya kisiasa na kijamii, ambayo wakati fulani yanaweza kuathiri uwezo wao wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuwajibika.

Sisi, wawakilishi wa nguvukazi ya walinzi wa pori na watetezi katika Kongamano la 10 la Walinzi wa Pori Duniani la IRF **TUNATOA MWITO** kwa serikali, waajiri wa walinzi wa pori, vyama vya walinzi wa pori, mashirika yasiyo ya kiserikali ya uhifadhi wa mazingira, wafadhili na washikadau wengine kuchukua hatua zifuatazo;

**KUTAMBUA WAJIBU**

*Licha ya jukumu lao muhimu, walinzi wa pori hawapati utambuzi wanaostahili na wanaohitaji, na kuna hitaji kubwa la;*

1. Kutetea kutambuliwa kwa taaluma za walinzi wa pori.
2. Kutambua na kuendeleza jukumu muhimu la walinzi wa pori katika kulinda na kutoa huduma za mfumo wa ikolojia muhimu kwa ustawi wa binadamu na ubora wa maisha.
3. Kuheshimu, kulinda na kutimiza haki za walinzi wa pori kulingana na kanuni na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.
4. Kutambua walinzi wa pori kama mmoja wa wasaidizi wa kwanza katika dharura zinazotishia maisha ya binadamu, wanyamapori au mali ndani na karibu na Maeneo Yanayolindwa na Kuhifadhiwa (PCA) na wahakikishe kuwa wanapewa maarifa, ujuzi, uwezo na zana zinazohitajika kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi na usalama.
5. Kutambua jukumu la walinzi wa pori katika kuzuia na ufuatiliaji wa magonjwa ya kuambukiza yanayoenea kati ya wanyama katika Maeneo Yanayolindwa na Kuhifadhiwa (PCA).
6. Kutambua ari ya walinzi wa pori na familia zao katika kujitolea kwao kwa dhati kulinda sayari yetu.
7. Kutetea kutambuliwa zaidi kwa jukumu la walinzi wa pori katika ulinzi na uhifadhi wa nchi kavu, maji ya bara, maeneo ya pwani na baharini.

Our funders

Institutional support

**MASHARTI**

*Huku tukizingatia matokeo ya Ripoti ya Hali za Walinzi wa Pori[3] na kutambua kwamba walinzi wa pori mara nyingi hufanya kazi kwa muda mrefu katika mazingira magumu na wakati mwingine hatari, ni muhimu;*

1. Kuhakikisha usalama wa kazi na afya ya walinzi wa pori kwa kutekeleza **Viwango vya Ajira na Ustawi Ulimwenguni**.
2. Kutetea uboreshaji wa mazingira ya kazi ya walinzi wa pori kupitia utekelezaji na ufuatiliaji wa mapendekezo ya Ripoti ya Hali za Walinzi wa Pori.
3. Kuanzisha na kukuza jukwaa la kimataifa chini ya IRF kwa ajili ya kupiga ripoti za vifo vya walinzi wa pori katika mazingira ya kazi.
4. Kutambua mapungufu ya kifedha katika baadhi ya nchi na kuhimiza jumuiya ya uhifadhi wa mazingira kujitahidi kupata mfumo unaofaa wa bima, inayostahili kwa walinzi wa pori.

**UMAHIRI**

*Kwa kuzingatia kuwa walinzi wengi wa pori duniani kote hawana ujuzi, vifaa na mafunzo yanayohitajika ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo[4], na kwa kuzingatia hitaji la dharura la kuongeza idadi na ufanisi wa maeneo yanayolindwa na kuhifadhiwa ili kufikia lengo la 30x30 la Mfumo wa Kunming-Montreal wa Bioanuwai Ulimwenguni[5], lazima:*

1. Tuhakikishe kwamba walinzi wote wa pori wanapata ujuzi na uwezo muhimu wa kiufundi unaowiana na **Umahiri wa Kimataifa wa Walinzi wa Pori**, ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, usalama na kuwajibika.
2. Tusaidie na tuwezeshe vyama vya walinzi wa pori kukuza na kurahisisha ufikiaji wa fursa muhimu za kujifunza kupitia mpango wa kujifunza wenyewe kwa wenyewe.
3. Tusaidie taasisi za mafunzo ya walinzi wa pori wa kikanda na kitaifa kutoa mipango ya kuwaimarisha inayokidhi mahitaji ya ndani na kuwiana na Umahiri wa Kimataifa wa Walinzi wa Pori.
4. Tukumbatie mifumo ya maarifa ya Watu wa Kiasili na Jumuiya za Mitaa (IPLC) katika usimamizi bora wa rasilimali asilia zinazoweza kutumiwa tena.
5. Tuhakikishe kwamba idadi ya walinzi wa pori wanaotumwa mahali pa kazi wanatosha kushughulikia mahitaji ya eneo na vitisho vinavyowakabili; ikiwezekana kuzingatia na kutilia maanani kanuni za kitaifa za idadi ya walinzi wa pori[6].

---

3 https://www.internationalrangers.org/state-of-the-ranger/
4 https://www.internationalrangers.org/state-of-the-ranger/
5 https://www.cbd.int/gbf/targets/3
6 https://www.nature.com/articles/s41893-022-00970-0

**NGUVUKAZI**

*Kwa kutambua jukumu muhimu la watu wa kiasili, jumuiya za mitaa, wanawake na makundi mengine yenye uwakilishi mdogo katika usimamizi wa maeneo yanayolindwa na kuhifadhiwa, kuna haja kubwa ya:*

1. Kushughulikia kikamilifu kukosekana kwa usawa wa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na uwakilishi wa wanawake[7] na Watu wa Kiasili na Jumuiya za Mitaa[8] katika sekta ili kuunda nguvukazi iliyo bora zaidi, pana na thabiti zaidi.
2. Kuboresha usawa katika upatikanaji wa ajira, fursa za kujiimarisha, mazingira bora ya kufanya kazi na maendeleo ya kikazi, bila kujali umri, jinsia, rangi, hadhi, tabaka, kabila, lugha, dini, mwelekeo wa kijinsia na ulemavu.
3. Kutambua, kukuza na kuunga mkono Watu wa Kiasili na Jumuiya za Mitaa kama walinzi wa pori na wasimamizi wa mazingira asili.
4. Kutoa nafasi salama kwa walinzi wa pori wanawake katika maeneo yao ya kazi, ikiwa ni pamoja na malazi salama na usaidizi wa kutosha wa ustawi[9].
5. Kuunga mkono na kutekeleza mipango za ushirikishaji na uhamasishaji wa vijana ili kuvutia vijana kuwa kizazi kijacho cha walinzi wa pori.

**MAADILI**

*Katika kutambua umuhimu wa uwajibikaji na kuchukua jukumu katika taaluma, ni muhimu:*

1. Kutambua na kukuza uadilifu wa walinzi wa pori ilivyoainishwa katika **Kanuni ya Maadili ya IRF** kwa washikadau wote.
2. Kuhakikisha ujumuishaji na utekelezaji wa Kanuni za Maadili za kina, zilizosanifishwa, zinazowiana na Kanuni za Maadili za IRF na kujitolea kuzuia utovu wa nidhamu kupitia Taratibu Maalum za Utendaji zinazoongoza maadili ya walinzi wa pori.
3. Kuimarisha uwajibikaji unaofaa na mifumo ya kutoa maoni kuhusu maadili ya walinzi wa pori, ikiwa ni pamoja na hatua za kupambana na rushwa.
4. Kukuza ufikiaji wa njia rahisi, salama na zinazoficha utambulisho ili walinzi wa pori wapige ripoti kuhusu tabia zisizo halali au zisizo za kimaadili.

[7] https://www.internationalrangers.org/resource/towards-gender-equality-in-the-ranger-workforce/
[8] https://escholarship.org/uc/item/2754m0kj
[9] https://www.internationalrangers.org/wp-content/uploads/Towards-Gender-Equality-In-The-Ranger-Workforce-SUMMARY.pdf

Our funders
Institutional support
Ranger sponsors

**MICHANGO YA WALINZI WA PORI**

*Katika kutambua* ***jukumu muhimu la walinzi wa pori*** *katika utekelezaji wenye ufanisi wa ahadi za kimataifa na utaratibu wa kifedha wa uhifadhi wa mazingira, kuna haja ya;*

1. Kutetea ushirikishaji wa vipengele mahususi vya walinzi wa pori katika Mfumo wa Kimataifa wa Bioanuwai wa Kunming-Montreal na Mikakati na Mipango ya Utekelezaji ya Kitaifa ya Bioanuwai (NBSAP).
2. Kutambua michango ya walinzi wa pori katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuafikiana, ustahimilivu, kupunguza hatari za maafa na kuweka ahadi za kimataifa za hali ya hewa.
3. Kuhakikisha kuwa walinzi wa pori wanashirikishwa kikamilifu na kuhusishwa katika mijadala ya bioanuwai na hali ya hewa ya kimataifa na michakato ya kufanya maamuzi ya uhifadhi wa mazingira kupitia taratibu zinazofaa.
4. Kuangazia na kuendeleza majukumu ya walinzi wa pori katika suluhu za kiasili, mikopo ya kaboni, mikopo ya bioanuwai, suluhu asili zenye faida ya kifedha na mbinu nyinginezo za ufadhili wa uhifadhi wa mazingira.
5. Kutambua michango ya walinzi katika kufikia Malengo Endelevu ya Maendeleo.

**ZAIDI YA HAYO, TUNATOA MWITO kwa halmashauri ya IRF kuandaa mpango ya kazi wa kutekeleza Azimio la Hyères la Walinzi wa Pori, 2024 kwa ushirikiano na mashirika yasiyo ya kiserikali, washirika, wafadhili na washikadau husika.**

Our funders

Institutional support

Ranger sponsors